**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**BODI YA HUDUMA ZA MAKTABA - ZANZIBAR**

# TANGAZO LA SHINDANO LA UANDISHI

Bodi Ya Huduma za Maktaba – Zanzibar inawakaribisha watunzi na waandishi wa kazi za kubuni za fasihi ya Kiswahili, kushiriki katika **Shindano la Uandishi -2024.** Shindano hili litahusisha kazi za ***Riwaya, Tamthilia***, ***Ushairi*** pamoja ***Hadithi za Watoto***. Mwandishi awasilishe utanzu mmoja tu atakaouchagua. Tanzu zaidi moja hazitopokelewa. Washiriki na Washindi wa shindano hili watazawadiwa zawadi nono kwa Lengo la kuendeleza tasnia ya utunzi na uandishi wa vitabu Zanzibar.

## VIGEZO VYA UANDISHI

### 1. KAZI ZA RIWAYA

a) Mshiriki awe Mzanzibari.

b) Mswada wa riwaya uwe katika lugha ya Kiswahili.

c) Mwandishi atalazimika kutuma kazi moja tu (mswada au kitabu)

d) Kitabu kiwe kimechapishwa kuanzia mwaka 2019 hadi 2024 na kisiwe kilishinda katika mashindano yoyote na kupata tuzo.

e) Ukubwa wa mswada wa riwaya uwe na maneno kati ya 60000 na 100000.

f) Sehemu yoyote ya mswada isiwe imenakiliwa kutoka katika riwaya yoyote.

g) Kitabu au mswada wa riwaya ambao ulishinda nafasi ya 1-3 katika mashindano ya tunzo nyingine zozote hauruhusiwi kutumwa katika shindano hili.

h) Mwandishi awasilishe mswada wenye uasili – yaani alioubuni mwenyewe.

i) Mswada utakaotumwa uwe umeandikwa vizuri na ujikite katika masuala ya muhimu kadhaa ya kuelimisha kijamii.

## 2. KAZI ZA USHAIRI.

a. Mshiriki awe Mzanzibari.

b. Ushairi au Utenzi uwe katika lugha ya Kiswahili.

c. Mwandishi atalazimika kutuma kazi moja tu (mswada au kitabu)

d. Kitabu kiwe kimechapishwa kuanzia mwaka 2019 hadi 2024 na kisiwe kilishinda katika mashindano yoyote na kupata tuzo.

e. Mswada wa mashairi uwe na mashairi yasiyopungua 50 na yasiyozidi 65. Kila shairi moja liwe na beti zisizozidi 15.

f. Mswada wa utenzi uwe na beti kati ya 300 – 450.

g. Sehemu yoyote ya mswada isiwe imenakiliwa kutoka katika mashairi yoyote au utenzi wowote.

h. Kitabu au mswada wa mashairi au utenzi ambao ulishinda nafasi ya 1-3 katika mashindano ya tunzo nyingine zozote hauruhusiwi kutumwa katika shindano hili.

i. Mwandishi awasilishe mswada wenye uasili – yaani alioubuni yeye mwenyewe.

j. Kitabu au mswada wa ushairi au utenzi ambao ulishinda nafasi ya 1-3 katika mashindano ya tunzo nyingine zozote, hauruhusiwi kutumwa katika shindano hili.

k. Mswada utakaotumwa uwe umeandikwa vizuri na ujikite katika masuala ya muhimu kadhaa ya kuelimisha kijamii.

## 3. KAZI ZA TAMTHILIYA.

a. Mshiriki awe Mzanzibari.

b. Kitabu au Mswada wa tamthiliya uwe katika lugha ya Kiswahili.

c. Mwandishi atalazimika kutuma kazi moja tu (mswada au kitabu)

d. Kitabu kiwe kimechapishwa kuanzia mwaka 2019 hadi 2024 na kisiwe kilishinda katika mashindano yoyote na kupata tuzo.

e. Uwe na kurasa kati ya 60 – 80.

f. Sehemu yoyote ya mswada isiwe imenakiliwa kutoka katika tamthiliya yoyote au igizo lolote la jukwaani.

g. Kitabu au mswada wa tamthilia ambao ulishinda nafasi ya 1-3 katika mashindano ya tunzo nyingine zozote hauruhusiwi kutumwa katika shindano hili.

h. Mwandishi awasilishe mswada wenye uasili – yaani alioubuni yeye mwenyewe.

i. Mswada utakaotumwa uwe umeandikwa vizuri na ujikite katika masuala muhimu kadhaa ya kuelimisha kijamii.

## 4. KAZI ZA HADITHI ZA WATOTO

a. Mshiriki awe Mzanzibari.

b. Kitabu au Mswada uwe katika lugha ya Kiswahili, rahisi na inayoeleweka.

c. Mwandishi atalazimika kutuma kazi moja tu (mswada au kitabu)

d. Uwe na maneno kati 250-1000

e. Kitabu kiwe kimechapishwa kuanzia mwaka 2019 hadi 2024 na **kisiwe** kilishinda katika mashindano yoyote na kupata tuzo.

f. Kitabu au Mswada wa hadithi ulenge watoto wa umri kati ya miaka 5 -12

g. Sehemu yoyote ya mswada isiwe imenakiliwa kutoka katika hadithi yoyote.

h. Kitabu au mswada utakaowasilishwa ni lazima uwe na michoro halisi(isinakiliwe kutoka katika mitandao).

i. Kitabu au Mswada utakaotumwa ujikite katika masuala  muhimu kadhaa ya kuelimisha watoto.

**TARATIBU ZA KUWASILISHA MSWADA AU KITABU**

a) Mswada utumwe kama kiambatisho kwa *Microsoft word*.

b) Ukurasa wa kwanza wa mswada uwe na kichwa cha mswada na jumla ya maneno kwa riwaya na hadithi za watoto, idadi ya kurasa kwa tamthiliya na  idadi ya mashairi au idadi ya beti kama ni utenzi.

c) Kitabu au mswada uwe na namba kwenye kila ukurasa.

*d)* 4. Maandishi yawe katika "*Times new Roman''* ukubwa wa herufi *(font size*) Uwe 12 na *double spacing.*

e) Mwandishi asiandike jina lake wala taarifa zake binafsi kwenye mswada au kitabu

f) Mwandishi atume mswada wake kwa kutumia barua pepe itakayoambatishwa na mswada. Kwenye barua pepe aandike majina matatu kwa ukamilifu, jinsia yake, namba ya simu,anuani, wasifu wake usiozidi maneno 100 na umri wake. (Inasisitizwa mwandishi asiweke taarifa hizi kwenye ukurasa wowote wa mswada au kitabu).

g) Kitabu au mswada uwasilishwe kati ya Juni 20 na Ogasti 1, 2024.

h) Tuma mswada wako wa nakala laini *(softcopy)* kwa njia ya kieletroniki kwa kutumia anuani ya barua pepe ifuatayo: ***mashindano@zls.go.tz***

**Kwa taarifa zaidi , wasiliana na:**
**BODI YA HUDUMA ZA MATABA ZANZIBAR**
**Mtaa wa Gymkhan-Maisara**
**SIMU: +255776792299**
**EMAIL:info.zlsb@zls.go.tz**